# CHUO KIKUU CHA SOKOINE CHA KILIMO

# SUA



## MATUKIO YA MWEZI JUNI - AGOSTI, 2020

*SUA yaibuka Mshindi Maonesho ya Nane Nane Kitaifa, 2020* *Uk.23*



*SUA yapongezwa kwa kusaidia mapambano dhidi ya COVID-19* *Uk. 22*

www.sua.ac.tz

SUA Yakabidhi mifuko mia moja ya saruji Shule ya msingi Mlali Uk.18

"ARDHI NI HAZINA"

# Hospitali ya SUA yapongezwa kwa huduma nzuri za Afya



*Aliyekuwa Mbunge wa viti maalumu kwa upande wa Vyuo Vikuu nchini Dkt. Jasmine Tisekwa (wa pili kushoto) mstari wa mbele akiwa kwenye picha ya pamoja na Makamu Mkuu wa Chuo Prof. Raphael Chibunda (wa pili, kulia), Prof. Yasinta Muzanila(wa kwanza kulia ) pamoja Wauguzi wa Hosptali ya SUA.*

Hospitali ya Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) imepongezwa kwa kuendelea kutoa huduma nzuri za Afya wakati wote.

Pongezi hizo zilitolewa na Mbunge wa viti maalumu kwa upande wa Vyuo Vikuu nchini Mhe. Dkt Jasmine Tiisekwa wakati alipokabidhi Mashuka 20 ya hospitali, ndoo nane kwa ajili ya kunawia, sabuni, pamoja na vyombo vingine vya usafi kwa hospitali ya SUA Kampasi Kuu siku ya Jumatatu tarehe 8, Juni, 2020.

"Nafahamu kuwa Hospitali hii ni muhimu sana na Jamii yote ya hapa Morogoro na hata nje ya Morogoro wanakuja hapa kutibiwa, pia nimeona juhudi zinazofanywa na Wahudumu wa hapa hivyo na mimi nimeona ni vyema kuja kuchangia chochote na niwashauri Wadau wengine kufanya kitu ili kusaidia Hospitali yetu iende vizuri" alisema Dkt Tiisekwa.

Alisema kama Kiongozi ameguswa na janga la virusi vya Corona linaloendelea duniani na amethamini mchango mkubwa wa SUA hivyo amerudi kulipa fadhila kwa kutoa msaada katika Kituo hicho cha Afya.

Naye Makamu Mkuu wa Chuo cha SUA Prof. Raphael Chibunda alimshukuru Dkt. Tiisekwa kwa msaada alioutoa na anaonesha ana mapenzi ya dhati kwa SUA yaliyopelekea kutoa msaada huo kama ilivyo kwa baadhi ya Wadau wengine waliopita katika Chuo hicho.

Aliongezea kuwa vifaa alivyotoa amevitoa katika kipindi muafaka kwa kuwa Chuo bado kinaendelea na mapambano dhidi ya Virusi vya Corona ingawa hali ya ugonjwa kwa sasa sio mbaya kama ilivyokuwa awali.

*Inatoka Uk. 1*

"Kama Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania anavyotusisitiza tuendelee kuchukua tahadhari dhidi ya Virusi vya Corona hivyo vifaa ulivyotuletea vitazidi kutujengea uwezo wetu kwenye kuchukua tahadhari lakini pia kwenye kuhudumia Jamii" alisema Prof. Chibunda

Kwa Upande wa Daktari Mkazi wa Hospitali hiyo Dkt. Omar Kasuwi alimshukuru Dkt. Tiisekwa kwa msaada huo lakini pia kwa kutambua mchango wa hospitali ya SUA na sekta ya afya kwa ujumla hususani katika kipindi hiki cha mapambano dhidi ya Virusi vya Corona kwani si wengi wenye moyo wa kutoa kama wake.




***Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) Prof. Raphael Chibunda (kulia) akipokea moja ya vifaa vya matibabu kutoka kwa aliyekuwa Mbunge wa Viti maalumu kwa upande wa Vyuo Vikuu nchini, Dkt Jasmine Tisekwa.***

***"Nafahamu kuwa Hospitali hii ni muhimu sana na Jamii yote ya hapa Morogoro na hata nje ya Morogoro wanakuja hapa kutibiwa, pia nimeona juhudi zinazofanywa na Wahudumu wa hapa hivyo na mimi nimeona ni vyema kuja kuchangia chochote na niwashauri Wadau wengine kufanya kitu ili kusaidia Hospitali yetu iende vizuri"***
***Dkt. Tisekwa***

# Kalobelo: Wakulima itumieni SUA ili kulima kwa tija na kuepuka migogoro



*Katibu Tawala Mkoa wa Morogoro Mhandisi Emmanuel Kalobelo akiongea na wananchi waliojitokeza katika maonesho ya siku ya wakulima, kwenye viwanja vya Shule ya msingi Mlali wilaya ya Mvomero, Morogoro.*

Wakulima Mkoani Morogoro wamesisitizwa kutumia ipasavyo Wataaluamu wa Kilimo kutoka Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) ili kupata elimu na mbinu sahihi na rahisi za Kilimo zitakazo wawezesha kulima kwa tija ili kuondokana na njaa na umaskini ikiwa ni pamoja na kuepuka migogoro ya ardhi

Hayo yalisemwa na Afisa Tawala Mkoa wa Morogoro Mhandisi Emmanuel Kalobelo wakati akifunga rasmi Maonesho ya siku tatu ya kilimo yaliyoandaliwa na Chuo Kiuu cha Sokoine cha Kilimo kwa kushirikiana na Shirika la RECODA yaliyofanyika siku ya alhamisi tarehe 2 Julai, 2020 kwenye uwanja wa mpira wa Shule ya msingi Mlali iliyopo Wilaya ya Mvomero.

Alisema kuwa Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) na Shirika la RECODA wamekuwa ni Wadau muhimu katika kutoa elimu kwa wakulima mkoani Morogoro. Wadau hao kwa kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Mvomero na Manispaa ya Morogoro wanatekeleza mradi unaotumia mfumo shirikishi ili kuleta mapinduzi ya kilimo unaofahamika kama RIPAT SUA unaozingatia mnyororo wa thamani ya mazao na ufugaji.

"Kwa kweli nakipongeza Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) na Shirika la RECODA kwa juhudi zao za kusambaza teknolojia hii rahisi kwa Wakulima wetu ambayo kwa macho yangu nimeshuhudia matokeo yake chanya katika mashamba Darasa yote tuliyopita na imeonekana kufanya kazi na kupokelewa kwa mikono miwili na Wakulima" alisema Mhandisi Kalobelo.

Alisema kuwa teknolojia hiyo ya RIPAT licha ya kuwa ni rahisi lakini pia ni njia sahihi ya wakulima

*Inatoka Uk. 3*

kuepukana na migogoro ya ardhi kwani teknolojia hiyo haihitaji mkulima kuwa na eneo kubwa zaidi ili kupata mazao mengi na badala yake kwa kufata mbinu rahisi na elimu itolewayo na wataalamu husika Mkulima ataweza kulima katika eneo dogo na kupata mazao ya kutosha.

"Nadhani sasa huu ni wakati sahihi wa wakulima kuachana na zana ya kung'ang'ania eneo kubwa kwa ajili ya kilimo kwa kudhani kuwa ndio njia sahihi ya kupata mazao mengi kitu ambacho si kweli na kime-kuwa kikipelekea migogoro ya mara kwa mara ya ardhi nchini" alisema Mhandisi Kalobelo.

Awali akiwa katika moja ya Shamba darasa, Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) Prof. Raphael Chibunda alimshukuru Afisa Tawala kwa kutenga muda wake na kujumuika nao katika zi-ara hiyo licha ya majukumu mengi aliyo nayo, ShIri-ka la RECODA ambao ni washirika wakuu wa SUA kwenye mafunzo ya mradi huo, pamoja na Ndaki ya Sayansi za Jamii na insia ambao ndio wa simamizi wa mradi huo kwa upande wa SUA na kuongeza kuwa SUA ipo tayali kushirikiana na wadau mbalimbali



*Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA ) Prof. Raphael Chibunda akizu-ngumza jambo wakati alipotembelea mashamba darasa yaliyopo Mlali Wilaya ya Mvomero, Morogoro*

***"Kwa miaka mingi sana Nchi yetu imekuwa ikiishi kwenye maigizo. Unakuta kama hivi wakulima wanaandaliwa , kamelimwa kabustani kadogo ka maonesho, wanahabari wanachukua picha na taarifa lakini baada ya hapo hakuna kinachoendelea tena kila kitu kinaishia hapohapo. Na kiukweli sisi kama Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo hatutaki kuwa sehemu ya maigizo hayo"***
***Prof. Chibunda***

*Inatoka Uk. 4*

katika kuleta maendeleo kupitia Wataalum wa kilimo waliopo chuoni hapo.
Prof. Chibunda alisema kuwa kama kuna kitu Serikali ya awamu ya tano chini ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. John Pombe Magufuli inakipinga na imefanikiwa kwa kiasi kikubwa ni maneno dhidi ya vitendo na maigizo yasiyo na tija kwa taifa letu.
"Kwa miaka mingi sana nchi yetu imekuwa ikiishi kwenye maigizo. Unakuta kama hivi wakulima wanaandaliwa, kamelimwa kabustani kadogo ka maonesho, wanahabari wanachukua picha na taarifa lakini baada ya hapo hakuna kinachoendelea tena kila kitu kinaishia hapohapo. Na kiukweli sisi kama Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo hatutaki kuwa sehemu ya maigizo hayo" Alisema Chibunda.
Alisema kuwa amefurahishwa na kauli mbiu ya maonesho hayo kuwa "njaa na umaskini kuwa historia inawezekana" lakini kwa kuzingatia mbinu sahihi za kilimo chenye tija pamoja na kuwashirikisha zaidi vijana ambao ni nguvukazi ya Taifa.
Naye Mratibu wa maonesho hayo ambaye pia ni Mhadhiri wa Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo Dkt Emmanuel Malisa alisema kuwa lengo kuu la mradi huo ni kuleta mapinduzi ya kilimo nchini kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wa kilimo kwa kusambaza teknolojia hiyo ya RIPAT ambayo itasaidia wakulima kujifunza mbinu mbalimbali za kilimo cha kisasa na chenye tija.
Dkt .Malisa aliongeza kuwa lengo lingine la mradi huo ni kuwafikia wakulima 720 ifikapo mwaka 2021 ambapo mbaka sasa zaidi ya wakulima 600 wameshafikiwa na mfumo na kizuri zaidi mfumo huo kwa sasa unafundishwa kwa Wanafunzi wa SUA ambao tunategemea mara baada ya kumaliza chuo watakwenda kusambaza elimu waliyopata kwenye maeneo mengine ya nchi.



***Katibu Tawala Mkoa wa Morogoro Mhandisi Emmanuel Kalobelo akiongea jambo na Wanakikundi cha Tukalegoya walio chini wa Mradi pamoja na baadhi ya Wadau wa Kilimo, wakati alipotembelea kwenye  Mashamba Darasa yaliyopo Mlali Wilaya ya Mvomero, Morogoro***

# Wanazuoni wampongeza JPM kwa kujenga SGR

Viongozi wakuu wa Vyuo Vikuu nchini wamei- pongeza Serikali ya Awamu ya Tano inayoongozwa na Rais Dkt. John Pombe Magufuli kwa kufanya maamuzi makubwa ya kujenga Reli ya mwendokasi (SGR) pamoja na Mkandarasi wa reli hiyo kwa kazi nzuri wanayoifanya Usiku na mchana ili kukamilisha reli hiyo kwa wakati.

Akiongea mara baada ya kutembelea Handaki Refu zaidi kati ya mahandaki yanayojengwa Mwenyekiti wa Kamati ya Makamu wakuu wa vyuo vyote vya Umma na Binafsi ambaye pia ni Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) Prof. Raphael Chibunda alisema ujenzi wa Reli hiyo utakuwa chachu katika kuleta maendeleo nchini.

Alisema lengo la ziara hiyo kama viongozi wa wasimamizi wa Vyuo Vikuu nchini ambavyo vinazalisha Wataalamu katika fani mbalimbali kwa maendeleo ya Taifa ni kujionea maendeleo ya mradi huo wa kipekee na wa iana yake Afrika Mashariki.

Prof. Chibunda alisema kupitia ziara hiyo sasa wanaweza kuona ni kwa namna gani wataweza kuzalisha Wataalamu ambao watasaidia kuendeleza na kuendesha Reli hiyo pale itakapokamilika lakini pia wamefarijika kuona vijana wengi wa kitanzania ambao ni wahitimu wa Vyuo vyetu wamepata ajira na wanavyoshiriki kujifunza ili kampuni hiyo ya ujenzi itakapoondoka waweze kuiendesha watanzania wenyewe na kufanya miradi mingine ya aina hiyo.

“ Sisi leo tunashukuru tumejionea wenyewe kwa



*Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) Prof. Raphael Chibunda akiongea na Waandishi wa Habari wakati wa Ziara ya Wakuu wa Vyuo Vikuu Tanzania, kwenye Ujenzi wa Reli ya mwendokasi (SGR)*

*Inatoka Uk. 5*

macho yetu na hapa tupo viongozi wakuu wa Vyuo 38 na wengine wameshindwa kufika kutokana na majukumu makubwa ya kiakazi hivyo tumeridhika na kufarijika na maendeleo ya mradi huu ambao unagharimiwa na fedha za kodi za Watanzania na sio wafadhili " Alisema Prof. Chibunda.

Naye Prof. Yohana Msanjila ambaye ni Makamu wa Mkuu wa Chuo Kikuu cha St. Johns cha Dodoma alisema hii ni hatua kubwa sana ya maendeleo ambayo Tanzania imepiga katika kufanikisha ujenzi huu Mkubwa wa Reli ambao utasaidia sana katika kuongeza kasi ya maendeleo.

"Mradi huu ukikamilika nakuhakikishia Tanzania itapiga hatua kubwa za haraka za maendeleo kutoka hapa tulipo sasa" Alisisitiza Prof. Msanjila.

Kwa upande wake Rasi wa Chuo Kishiriki cha Mkwawa Iringa Prof. Esther Dungumaro alisema kujenga mradi huu ni uthubutu wa hali ya juu kwa Serikali ya awamu ya tano kwenye kujenga Miradi mikubwa ya aina hii ambao umetumia fedha nyingi sana.

"Nampongeza sana Rais wetu Dkt. John Pombe Magufuli kwa kutekeleza mradi huu kwa fedha za Tanzania na nina amini kwa uthubutu huu tunaiona Tanzania ya kipekee sana kimaendeleo" Alisema Prof. Ester.

Naye Katibu Mtendaji wa Tume ya Vyuo Vikuu Prof. Charles Dominick Kihampa aliwapongeza viongozi hao wa Vyuo Vikuu Nchini kwa kuamua kutembelea Mradi huo na kuona wahitimu kutoka kwenye Vyuo vyao wanavyoshiriki katika ujenzi na kuona ni kwa namna gani wanavyoweza kuboresha Elimu wanayoitoa ili kuendana na mahitaji ya soko." Zipo sehemu nyingi ambazo watanzania wataweza kunufaika kupitia Mradi huu wa Reli lakini nimefarijika sana kama msimamizi wa ubora wa elimu vyuoni kuona viongozi hawa wa Vyuo wametembelea Mradi huu maana sasa wataweza kuona aina za programu wanazoweza kuanzisha ili utakapokamilika tuwe na watanzania ambao wataweza kutekeleza miradi mingine kama hii mikubwa ambayo nchi yetu itahitaji kuijenga" alisisitiza Prof. Kihampa.






Prof. Faustine Karrani ambaye ni Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Dodoma UDOM alisema kazi hii iliyofanywa na Serikali ya awamu ya tano ni kazi nzuri na kubwa na yenye faida kubwa kiuchumi na kijamii hasa katika kuimarisha usafirishaji na uchukuzi nchini katika historia ya nchi yetu.

" Tumefurahishwa kwa hatua hii kazi hii ni kubwa na zuri na tunaamini utakapokamilika utaleta mageuzi makubwa sana kwa nchi yetu ya Tanzania" Prof. Karrani.

# SUA yaandaa sera ya kudhibiti udhalilishaji wa kingono



*Rasi wa Ndaki ya Kilimo Prof. Benard Chove akizungumza na washiriki wakati wa Warsha ya kujadili Rasimu ya sera ya kudhibiti udhalilisha wa kingono.*

Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA)Kimeandaa Warsha ya Siku moja na Wadau mbalilmbali Chuoni hapo ili kujadili Rasimu ya Sera ya kudhibiti Udhalilishaji wa Kingono yenye la kutatua changamoto ya udhalilishaji huo katika maeneo ya Chuo.
Akifungua Warsha hiyo Leo Siku ya Jumatano tarehe 8 Julai, 2020 iliyofanyika katika ukumbi wa ICE Kampasi Kuu kwa niaba ya Makamu wa Mkuu wa Chuo Kaimu wa Rasi wa Ndaki ya Kilimo Prof. Bernard Chove alisema Sera hiyo ni muhimu hususani katika kipindi hiki ambacho Serikali imeanza kuchukua hatua dhidi ya udhalilishaji huo wa kingono katika maeneo mbalimbali ya nchi hususani Vyuoni.
Prof. Chove aliwataka wadau wanaoshiriki kwenye Warsha hiyo kutoa maoni yatakayosaidia kuboresha Sera hiyo ili ilete manufaa kwa Chuo na umma kwa ujumla.
"Maoni hayo yatasaidia sana kuboresha Sera hii na kusaidia kuimarisha mifumo yetu ya kudhibiti Udhalilishaji wa kingono miongoni mwa Wafanyakazi, Wanafunzi na wadau wengine wa Chuo", alisema Prof. Chove.
Kwa upande wake Mhadhiri Mwandamizi kutoka Ndaki za Sayansi Jamii na Insia Dkt. Fatihiya Massawe Mkuu wa Mradi mdogo wa namna ya kufanya mazingira ya kazi kuwa salama kutokana na Udhalilishaji wa kingono alisema Sera hiyo itakapokamilika



*Rasi wa Ndaki ya Kilimo Prof. Benard Chove (katikati) waliokaa, Rasi wa Ndaki ya Sayansi ya Jamii na Insia Dkt Samwel Kabote na Mhadhiri Mwandamizi kutoka Ndaki za Sayansi ya Jamii na Insia Dkt. Fatihiya Massawe wakiwa katika picha ya pamoja na Washiriki wa Warsha ya kujadili Rasimu ya Sera ya kudhibiti Udhalilishaji wa kingono*

*Inatoka Uk. 8*

itawasaidia watu kupata uelewa wa namna ya kujikinga na udhalilishaji wa kingono.

"Matarajio yetu Sera hii itakapokamilika suala la Unyanyasanyaji na Udhalilishaji wa Kingono halitakuwepo tena kwa sababu Wanafunzi, Wafanyakazi na wadau wengine hapa Chuoni watapata elimu ya kutosha ya namna bora ya kutoa taarifa kuhusu vitendo vya aina hiyo na hivyo kuweza kufanyiwa kazi kwa mujibu wa matakwa ya Sera na sheria za Utumishi wa Umma", alisema Dkt Fatihiya

Mradi mdogo wa namna ya kufanya mazingira ya kazi kuwa salama kutokana na Udhalilishaji wa kingono unafadhiliwa na Wakfu wa HIVOS wenye Makao yake Makuu nchini Kenya na unatekelezwa na watumishi watano na mwanafunzi mmoja wa Chuo kutoka SUA ambapo washiriki wa mradi huo wanajumuisha wafanyakazi wanataluma, wafanyakazi waendeshaji na wanafunzi.

Wakati akifunga Warsha hiyo Rasi wa Ndaki Sayansi ya Jamii na Insia Dkt. Samweli Kabote aliwapongeza watekelezaji wa Mradi walioibua wazo hilo la kuandaa Sera ya kudhibiti Udhalilishaji Unyanyasaji wa Kingono Chuoni na kuongeza kuwa anatumaini maoni yatakayotolewa yatasaidia na kumaliza kabisa Unyanyasaji wa Kingono katika Chuo cha SUA.

# NMB yaipongeza SUA kwa kuwa na wahitimu bora

Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) Prof. Raphael T. Chibunda ameishukuru Benki ya NMB kwa kufanya maamuzi mazuri ya kuichagua SUA na kuendesha Programu ya Kuandaa Wahitimu kuwa Wafanyakazi wenye usanifu mkubwa wanapokuwa makazini.

Akizungumza wakati wa ufunguzi wa program hiyo ya siku moja (Career Fair Day) iliyoandaliwa na Benki ya NMB pamoja na SUA iliyofanyika sku ya jumamosi tarehe 11 Julai, 2020 katika ukumbi wa Freedom Square Kampasi ya Solomon Mahlangu- SUA Prof. Chibunda aliihakikishia NMB kuwa wamefanya jambo sahihi.

“Mmefanya uamuzi mzuri kukichagua Chuo cha SUA kwani baadhi ya Taasisi kama Kampuni ya sukari pamoja na Kampuni ya Sigara (TCC) waliochukua Wahitimu wa SUA na wamewasifia kuwa wanauwezo mkubwa wa kufanya kazi,waaminifu na kufanya kazi kwenye Taasisi husika kwa kipindi kirefu bila kwenda Taasisi nyingine”, Alisema Prof. Chibunda.

Pia aliongeza kuwa mwaka jana Wizara ya Fedha iliajiri wanafunzi waliosoma Kilimo Biashara na kupata alama ya kuanzia 3.8 ambapo kati ya Waajiriwa 54 walioajiriwa, Waajirwa 38 walitoka SUA.

Naye Bw. Baraka Ladislaus Meneja wa Benki ya NMB Kanda ya Morogoro ambaye pia ni Muhitimu wa SUA mwaka 2004 wa shahada ya kwanza ya Sayansi ya Kilimo aliishukuru SUA kwa kumuandaa vizuri pamoja na kwamba kozi aliyosomea SUA sio anayoifanyia kazi Benki ila SUA imempa kujiamini na kuomba nafasi ilipotangazwa kwenye Benki hiyo.

“Tangu nianze kufanya kazi Benki ya NMB ni mwaka




*Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) Prof. Raphael Chibunda akiongea wakati wa ufunguzi wa Programu ya Kuandaa Wahitimu kuwa Wafanyakazi wenye usanifu mkubwa wanapokuwa makazini iliyoandaliwa na Benki ya NMB*

*Inatoka Uk. 10*

wangu wa 16, na tunapokuwa katika kazi tunakuwa kila baada ya muda mfano mimi niliajiriwa kama Afisa Mikopo lakini sasa ni Meneja na bado nina uhakika wa kufika nafasi nyingine zaidi ya hii hivyo nawashauri wahitimu tumieni fursa vizuri zinapotolewa mahali popote bila kuogopa," alisema Bw. Ladislaus.

Kwa upande wake Mratibu wa Programu hiyo Bi. Joanita R. Mlengo Mkuu wa kitengo cha Rasilimali Watu upande wa Taaluma kutoka Benki ya NMB alisema kuwa katika Benki ya NMB Waajiriwa wengi wanatokea SUA na wamekuwa wakifanya kazi vizuri hivyo wameona ni vema kuja kuongea na Wahitimu wa Chuo cha SUA na kuwapa fursa kuomba nafasi hiyo.

Aliongeza kuwa Programu hiyo ya kuwaandaa Wahitimu kwa kuwafundisha namna ya kufanya kazi huwa ni ya muda wa miaka miwili kisha inawaajiri, amewataka Wahitimu wa SUA kutumia vizuri fursa hii waliyoipata na kuomba kwa wingi ifikapo tarehe 20 Julai, 2020 kwani si Vyuo vyote vimepata nafasi hiyo ni Chuo cha DODOMA na Chuo cha SUA tu.

Mmoja wa wanafunzi waliofaidika na Programu hiyo Bw. Nsolo Mlozi Meneja wa NMB kanda ya kati Singida, Dodoma na Manyara ambaye pia ni muhitimu wa Chuo cha SUA mwaka 2006 wa Shahada ya Uchumi alisema kuwa anajivunia sana Chuo cha SUA kwani kimemjenga kwenye misingi mizuri ya Uongozi kwani alipokuwa SUA alikuwa Waziri wa Michezo na Waziri wa Starehe na kuwa mwenye kipaji bora.

Bw. Nsolo Aliwataka Wahitimu kutumia fursa zinazotokea mahali popote itawaongezea uwezo na uzoefu na hata wale wanaoendelea na masomo kutumia vipaji vyao vizuri wanapokuwa Chuoni.

Akihitimisha Programu hiyo Rais wa wanafunzi Bw. Mbalamwezi Ismail alishukuru Menejimenti ya SUA na Benki ya NMB kwa upendeleo walioupata kwa kupewa fursa hiyo na kuahidi kuichangamkia na kuwataka wahitimu wote kutopuuzia nafasi hiyo.



***Washiriki wakifatilia kwa umakini yanayoongelewa wakati wa Warsha ianyohusu programu ya kuandaa Wahitimu kuwa Wafanyakzi wenye usanifu mkubwa wanapokuwa kazini iliyoandaliwa na Benki ya NMB***

# Prof. Kabudi ameipongeza SUA kwa kazi nzuri



*Waziri wa Mambo ya nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki Mhe. Prof. Palamagamba Kabudi akiwa ameshika kikapu chenye mbogamboga, alipotembelea Mabanda ya SUA wakati wa uzinduzi wa Maonesho ya Wakulima nchini (Nane Nane) Morogoro, 2020*

Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki Mhe. Prof. Palamagamba Kabudi amepongeza kazi inayofanywa na Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo SUA katika kuboresha Kilimo, Mifugo na Uvuvi ili kuleta tija kwa Taifa.

Mhe. Prof. Kabudi alisema hayo alipotembelea Banda la SUA katika maonesho ya Nanenane kanda ya mashariki Agusti 1, 2020 kabla ya kwenda jukwaani kuzungumza na wananchi, waoneshaji na wadau wengine wa Kilimo wakati wa ufunguzi wa maonesho hayo.

"Chuo Kikuu cha SUA mnafanya kazi nyingi na nzuri kwa faida ya nchi lakini niwaombe muongeze jitihada za kutangaza kazi hizi ili watu wazijue na kunufaika nazo maana zinahitajika sana na Wakulima, Wafugaji na Wavuvi, alisisitiza Mhe. Prof. Kabudi. Alisema kuna kila sababu ya SUA kuona umuhimu wa kuanzisha mashamba ya Miti dawa badala ya kutegemea kuvuna porini hivyo ziwepo jitihada za makusudi za kuhamasisha watu kupanda akitolea mfano nchi kama Madagaska ambao wameanza kutoa Miti Dawa porini badala yake wamepanda mashamba makubwa na sasa wanauza na kuipatia

***Inatoka Uk. 12***

nchi hiyo dola 14 kwa mwaka.

Alisema anashukuru kwenye Ilani hii mpya ya Chama cha Mapinduzi kimeingiza mpango huo wa kuanzisha kiwanda kikubwa cha miti dawa hivyo ni muhimu kuanza kufikiria huko ili kujihakikishia miti dawa ya kutosha kiwanda hicho kitakapoanzishwa.

Mhe. Prof. Kabudi alifurahi kusikia kwa mara ya kwanza kuwa SUA ndio yenye Hospitali pekee ya Taifa ya Rufaa ya Wanyawa na Kwamba hili ni jambo kubwa ambalo Watanzania wanapaswa kulijua na kuitumia kikamilifu.

Kwa Upande wake Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo SUA Prof. Raphael Chibunda alimuonesha Mgeni Rasmi Prof. Kabudi matrekta kumi ambayo SUA imepewa na Mhe. Rais Dkt. John Pombe Magufuli na kusema kuwa yamekuwa chachu ya kuongeza mengine na vifaa mbalimbali vya kulimia na kufundishia kutokana na mapato ya ndani ya Chuo hicho




***Waziri wa Mambo ya nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki Mhe. Prof. Palamagamba Kabudi (wa pili kutoka kushoto mstari wa mbele) akisikiliza maelezo toka kwa Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Sokoine Prof. Raphael Chibunda wakati wa maonesho ya Nane Nnane mkoani Morogoro, 2020***

***“Chuo Kikuu cha SUA mnafanya kazi nyingi na nzuri kwa faida ya nchi lakini niwaombe muongeze jitihada za kutangaza kazi hizi ili watu wazijue na kunufaika nazo maana zinahitajika sana na Wakulima, Wafugaji na Wavuvi” Prof. Kabudi***

# Wakulima washauriwa kutumia bundi kudhibiti panya mashambani




*Dkt. Georgies Mgode akitoa maelezo kuhusu matumizi ya Bundi katika kulinda mazao shambani kwa Gavana wa Fedha Prof. Florens Luoga alipotembelea banda la SUA katika Maonesho ya Nane Nane Kitaifa Nyakabindi, Simiyu.*

Wakulima wameshauriwa kutumia ndege aina ya bundi ili kukabiliana na wanyama wadogo pamoja na wadudu waharibifu wa mazao shambani.
Akizungumza wakati wa Maonesho ya Nane Nane Dkt.Georgies Mgode, Mtafiti kutoka Kituo cha Kudhibiti Viumbe Hai Waharibifu katika Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) alisema tofauti na imani iliyojengeka kwa wengi kuhusu ndege aina ya bundi kuwa anatumika katika shughuli za kishirikina bundi akitumiwa vizuri anaweza kuwa mkombozi wa wakulima kwa kusaidia kupunguza panya na wadudu waharibifu wanaoharibu mazao shambani.
“Bundi ana uwezo mkubwa wa kuona wakati wa usiku hivyo huwinda wanyama wadogo wadogo kama panya, wadudu na hata ndege”, alisema Dkt. Mgode.
Dkt. Mgode aliongeza kuwa bundi wanapenda kula panya hivyo wanapokuwa mashambani kwa wingi wanapunguza kwa kiasi kikubwa wingi wa panya ambapo kwa siku moja bundi ana uwezo wa kula wastani wa panya kumi na mbili (12).
“Baadhi ya aina za bundi huishi kwa makundi na kuwinda kwa makundi kwa pamoja hivyo ndani ya msimu mmoja kundi moja la bundi linaweza kula mamia ya panya wadogo kwahiyo bundi wanaweza kudhibiti panya kirahisi na kumsaidia mkulima kupunguza matumizi ya kemikali mashambani”, alisema Dkt. Mgode.
Akielezea kuhusu namna ya kuwafanya bundi wavutiwe na kuzaana kwa wingi Dkt. Mgode alisema kuwa bundi wanahitaji kutengenezewa mazingira mazuri

*Inatoka Uk. 14*



kama vile kujengewa viota kwaajili ya kuishi na nguzo kwaajili ya kusimama nyakati za usiku wanapokuwa wanawinda.
"Viota vinaweza kutengenezwa mithili ya masanduku na kuning'inizwa kwenye miti au nguzo lakini mahali ambapo pana miti ya kutosha hapana haja ya kutengeneza viota", alisema Dkt. Mgode.
Bundi ni aina ya ndege ambaye hula nyama na hufanya mawindo wakati wa usiku na kupumzika wakati wa mchana. Kuna takribani aina 200 za Bundi ambapo wengi wao hupenda kuishi peke yao na kutafuta chakula ambapo huwinda wanyama wadogo wadogo kama panya, wadudu na hata ndege.

# Mpina avutiwa na maabara ya udongo inayotembea

Waziri wa Mifugo na Uvuvi Mhe. Luhaga Mpina amevutiwa na uwepo wa Maabara ya Udongo inayotembea ili kusaidia wakulima kupima afya ya udongo.
Akizungumza baada ya kutembelea banda la SUA katika Maonesho ya Nane Nane, viwanja vya Nyakabindi, leo tarehe 6 Agosti, 2020, Mhe. Mpina alisema ametembelea banda la Wizara ya Kilimo pamoja na TARI na kukuta kilio kikubwa kilichopo ni Maabara ya Udongo.
"Maabara ya udongo inaonekana ni kama kitu cha anasa lakini kwa vyovyote vile tunahitaji kupima afya ya udongo ili tuweze kuongeza uzalishaji wetu katika mazao ya kilimo." Alisema Mhe. Mpina.
Aidha, aliongeza kuwa maabara inayotembea ina gharama ndogo sana lakini inaweza kuhudumia Tarafa ama Wilaya nzima.
"Uzuri nimeambatana na Naibu Waziri wa Kilimo hivyo tutaangalia ni jinsi gani kwa kushirikiana na Wizara ya Kilimo pamoja na TAMISEMI ili Halmashauri zote walau wawe na hizi Maabara zinazotembea ambazo zitawezesha ardhi zetu kupimwa wakati wote katika mashamba ya wakulima wote", aliongeza Mhe. Mpina.
Mhe. Mpina alisema SUA ina mambo mengi mazuri ikiwemo Teknolojia ya kuhifadhi chanjo kwenye chombo kinachotengenezwa ambacho kinatumia gharama ndogo sana ukitofautisha na vifaa tulivyozoea na vingine kuhitaji matengenezo makubwa ama umeme ukizingatia sio kila eneo la wafugaji lina umeme.
Naye Naibu Waziri wa Kilimo Mhe. Hussein Bashe alisema kuwa anaishukuru SUA kwa kukubali kutumia maabara zake ya Udongo, Maabara ya Afya ya mbegu na Maabara ya Bayoteknolojia kuwezesha Maabara za Kilimo kutambulika Kimataifa ili kuweza kutoa huduma za kimaabara kwa ajili ya maendeleo ya Kilimo.
Pia aliiomba SUA ishirikiane na Wizara ya Kilimo, TARI pamoja na Halmashauri kushirikiana na kuhakikisha Maabara hizo za udongo zinazotembea zinapatikana.
Hadi sasa SUA imeweza kutoa maabara ya udongo inayotembea katika Halmasahauri ya Mvomero na tayari kuna mpango wa kupeleka katika Wilaya ya Njombe Mji na Mbeya Mjini.



*Waziri wa Mifugo na Uvuvi Mhe. Luhaga Mpina (kulia) akipata maelezo juu ya maabara ya udongo inayotembea toka kwa Wataalamu wa kilimo wa SUA wakati wa Maonesho ya Nane Nane Kitaifa mkoani Simiyu, 2020.*

# Wanafunzi Nyakabindi:Tafiti zinazofanywa SUA ni za kushangaza na zenye manufaa



Wanafunzi wa shule ya msingi Nyakabindi, Bariadi mkoani Simiyu wamesema tafiti zinazofanywa na Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo SUA ni za kushangaza na zenye manufaa kwa wakulima na watanzania kwa ujumla

Wakizungumza na kwenye viwanja vya maonesho ya wakulima Nanenane mkoani Simiyu, Kaka Mkuu wa Shule hiyo Kulwa Kubala na Dada Mkuu wa shule hiyo Marietha Masunga walisema wameshangazwa na uwezo wa panya katika kusaidia zoezi la kutambua sehemu ambayo ina bomu ili liteguliwe lakini pia panya wanavyotumika kunasa na kutambua makohozi yenye vimelea vya Kifua Kikuu

Akifafanua zaidi Kubala alisema katika hali ya kawaida wakulima wengi hawajui kuwa panya wanaweza kuwa na uwezo wa kufanya mambo hayo na wanachojua ni kuwa panya wao ni waharibifu tu na hasa kwa kula mazao mbalimbali kama mahindi yakiwa yanaota au mpunga unapokuwa shambani

"Nimepata mafunzo ya namna panya wanavyoweza kutumika katika kutambua na kujua wapi bomu lipo ili liondolewe lakini pia nimejifunza namna ambavyo unaweza kutumia panya kutambua makohozi yenye vimelea vya Kifua Kikuu", alisema Kubala

Akitoa maeelezo kwa wanafunzi hao waliofika katika banda la SUA Mtafiti kutoka Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo SUA Dkt. Georgies Mgode alisema pamoja na kuwepo kwa faida za panya kutumika kama kitoweo, kutambua eneo ambalo linakuwa na bomu na kutambua makohozi yenye vimelea vya kifua kikuu lakini pia kuna jamii za panya ambao ni waharibifu

"Kuna aina ya panya ambao ni waharibifu ambao panya mmoja tu anaweza kula gramu 8 hadi kumi kwa siku kwa hiyo mwaka una siku 365 ukizidisha mara kumi maana yake atakula zaidi ya gramu 300, maana yake ni kwamba panya mmoja mdogo yule anaweza kula kilo 3.5 sasa wakiwa 100 je? Na ndiyo maana tunasema kuwa panya ni waharibifu pamoja na faida zake" alisema Dkt. Mgode




***Dkt. Georgies Mgode akitoa maelezo ya tafiti mbalimbali zinazofanywa na Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo kwa Wanafunzi wa Shule ya Msingi Nyakabindi, Simiyu wakati wa Maonesho ya Nane Nane, 2020***

# SUA yakabidhi mifuko mia moja ya saruji kwa Uongozi wa Shule ya msingi Mlali

Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) kimekabidhi mifuko mia moja ya saruji yenye thamani ya shilingi milioni moja na nusu kwa ajili ya kuendeleza ujenzi wa vyumba 9 vya madarasa katika shule ya msingi Mlali iliyopo wilayani Mvomero mkoani Morogoro ambayo kwa muda mrefu imekuwa ikabiliwa na changamoto ya upungufu wa madarasa.

Akikabidhi mifuko hiyo kwa Mwalimu Mkuu wa Shule hiyo kwa niaba ya kamati ya ujenzi, siku ya Alhamisi tarehe 13 Agosti, 2020 Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu Cha Sokoine Cha Kilimo (SUA) Prof. Raphael Chibunda alisema Chuo kimeguswa na hali iliyopo shuleni hapo mara baada ya kuona wanafunzi wanasomea chini ya mti.

"Serikali imekuwa ikifanya jitihada za dhati ili kuboresha majengo ya Shule za Msingi, Sekondari na Vyuo lengo likiwa ni kuweka mazingira bora kwa Mwanafunzi kuweza kujifunzia na Mwalimu kufundishia hivyo sisi kama SUA tumetambua kazi kubwa inayoendelea kufanywa na Serikali ya awamu ya tano na tumeona ni vyema kuchangia kile kidogo tulicho nacho kwani tatizo hili la upungufu wa madarasa sio la wananchi wa Mlali tu bali ni letu sote" alisema Prof. Chibunda.




*Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) Prof. Raphael Chibunda (wa pili kulia) akikabidhi Mifuko ya Saruji kwa uongozi wa Shule ya Msingi Mlali Wilaya ya Mvomero, Morogoro*

*Inatoka Uk. 18*

Aidha aliitaka kamati ya ujezi shule ya Msingi Mlali kuakikisha inasimamia vyema matumizi ya Saruji hiyo ili iweze kutumika kama ilivyo pangwa na kuhakikisha Madarasa hayo yanakamilika kwa wakati ili wanafuzi wapate mahala pa kujifunzia.

Pia Prof. Raphael Chibunda aliwaahidi viongozi wa shule hiyo kuendelea kushirikiana nao katika kuhakikisha miundo mbinu ya shule inakamilika na kwamba walichotoa leo ni mwanzo na pindi wapatapo nafasi nyingine wataendelea kuisaidia shule hiyo.

Akizungumza mara baada ya kupokea msaada huo Mwalimu Mkuu wa Shule hiyo ya msingi Mlali Mwl. Omary Kibukila alikishukuru Chuo Kikuu cha Sokoine Cha Kilimo (SUA) kwa kutoa msaada huo na kuahidi Saruji hiyo kutumika kama inavyotakiwa.

Mwl. Kibukila alisema Shule hiyo inakabiliwa na upungufu wa madarasa 35 kati 43 yanayoitajika na mpaka sasa madarasa yanayotumika yakiwa ni nane tu, huku upungufu wa vyoo katika shule hiyo ukiwa ni matundu 35 kati ya 41 yanavyohitajika kwa wavulana na upande wa wasichana matundu 51 kati ya 60.

Kwa upande wake Afisa Elimu Kata ya Mlali Mwl. Ally Mbaraka alisema baada ya kuona changamoto hiyo ya upungufu wa madarasa katika shule hiyo Serikali ya Kijiji pamoja na Kata ilijipanga na kuanza ujenzi wa vyumba vya madarsa matatu ambayo yanatarajiwa kukamilika ifikapo mwezi wa tisa mwaka huu.

Pia aliongeza kuwa Halmashauri ya Wilaya ya Mvomero imeishaweka mpango wa kujenga vyumba vya Madarasa tisa ifikapo mwezi Novemba, 2020 huku Serikali Kuu ikiwa tayari imeleta kiasi cha Shilingi Milioni 40 ambazo zitatumia kukamilisha ujenzi wa madarasa pamoja na kuweka Madawati.



***Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) Prof. Raphael Chibunda akiwa katika picha ya pamoja na baadhi ya Wanafunzi wa Shule ya Msingi Mlali***

# SUA yakabidhiwa mashine za kusaidia kupumua ili kukabiliana na ugonjwa wa COVID-19



*Daktari Mkazi wa Hospitali ya Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) Dkt Omary Kasuwi (wa pili toka kulia) akipokea Mashine ya kusaidia kupumua ili kukabiliana na ugonjwa wa COVID-19, toka kwa Uongozi wa Kiwanda cha Tumbaku cha Alliance One Tobacco cha Morogoro*

Uongozi wa kiwanda cha Tumbaku mkoani Morogoro (Alliance One Tobacco) kimetoa mashine mpya nne za kusaidia kupumua (Oxygen) kwa hospitali ya Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) ili uunga mkono jitihada za Serikali katika kupambana na Ugonjwa wa COVID 19 .

Akikabidhi mashine hizo Mkurugenzi wa rasilimali watu wa Kiwanda hicho Bw. Blasius Lupenza alisema lengo la kutoa mashine hizo ni katika kuongeza jitihada za kupambana na ugonjwa wa Covid 19 na kwamba ijapokuwa tayari Mungu amelisaidia taifa letu kuepukana na ugonjwa huo ni lazima jitihada za kibinadamu ziendelee.

‘’Hizi mashine za kusaidia kupumua zitasaidia Jamii inayotuzunguka hapa Morogoro na watu wengine mbalimbali wanaofika kwenye hospitali hii wakiwa na hiyo shida ili afya za Watanzania ziendelee kuwa salama maana vifaa hivi vinahitajika sana kwenye kuokoa maisha ya watu wenye maambukizi ya virusi vya Corona ambao wapo katika hali mbaya kwa kushindwa kupumua” Alifafanua Bw. Lupenza.

Akizungumzia sababu ya wao kuchagua kupeleka mashine hizo kwenye hospitali ya SUA Bwana Lupenza alisema Hospitali ya SUA katika kipindi chote cha mlipuko wa ugonjwa huo imefanya kazi kubwa sana katika kusaidia kutibu na kuokoa maisha ya wagonjwa wa COVID 19, lakini pia miundombinu mizuri ingawa ina vifaa vichache hivyo vifaa vilivyotolewa vitasaidia

*Inatoka Uk. 20*

kuongeza jitihada za kuokoa maisha ya Watanzania wengi zaidi.

Akizungumza mara baada ya kupokea vifaa hivyo Daktari mkazi wa Hospitali ya SUA Dkt. Omary Kasuwi aliushukuru uongozi wa Kiwanda hicho kwa kuona umuhimu wa kutoa mashine hizo kwenye hospitali hiyo na kusema kuwa vifaa hivyo ni moja kati ya mahitaji muhimu kwenye jitihada za kupambana na ugonjwa wa COVID 19.

Dkt. Kasuwi alisema pamoja na kwamba kuna utulivu kidogo kwenye ugonjwa huo hapa nchini kama ambavyo viongozi wakuu wa Serikali wanavyoeleza lakini wamekuwa wakisisitiza jamii kuchukua tahadhari zote kwani sio kwamba ugonjwa umeisha kabisa hivyo kupata vifaa hivi ni moja ya muendelezo wa kuchukua tahadhari zinazotolewa na Serikali.

''Mpango huu wa kupata vifaa hivi leo umeanza miezi mitatu iliyopita ambapo umepitia katika hatua mbalimbali za mazungumzo na tathimini ya mahitaji lakini tunashukuru kuona leo tunakabidhiwa vifaa hivi muhimu kwenye hospitali yetu na kutuongezea uwezo zaidi wa kutoa huduma kwa wahitaji" Alisema Dkt. Kasuwi.

Tangu kulipuka kwa ugonjwa huo Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo SUA kimefanya jitihada kubwa katika mapambano dhidi ya ugonjwa huo ambapo hospitali ya SUA imeshiriki kikamilifu kusaidia kutibu na kuokoa maisha ya wagonjwa wa COVID-19 lakini pia maabara ya SUA iliyopo kwenye Ndaki ya Tiba za Wanyama za Sayansi za Afya iliteuliwa kuwa moja maabara zilizotumika katika kufanya uchunguzi wa sampuli za watu wanaohisiwa kuwa na Ugongwa wa Covid 19 nchini.



# SUA yapongezwa kusaidia mapambano dhidi ya COVID-19

Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii Jinsia Wazee na Watoto Mhe. Ummy Mwalimu amekishukuru Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) na Wataalamu wake kwa msaada Mkubwa waliotoa katika mapambano dhidi ya Ugonjwa wa COVID 19.
Mhe. Mwalimu aliyasema hayo alipotembelea Banda la SUA kwenye maonesho ya Wakulima nanenane Kanda ya Mashariki yaliyofanyika Mkoani Morogoro kabla ya kufunga rasmi maonesho hayo Kikanda.
"Nitumie nafasi hii kuushukuru Uongozi mzima wa SUA na Watafiti wake kwa msaada mkubwa mliotoa wakati wa mapambano ya COVID 19 Kwa kusaidia kwenye upimaji wa sampuli mbalimbali za wagonjwa kwa ubora mkubwa, Hakika tuna kila sababu ya kuwashukuru kwa jitihada hizi kubwa mlizozifanya" alisisitiza Mhe. Ummy Mwalimu.
Aliongeza "Wakati tunahangaika na zoezi la upimaji wa sampuli zilizokuwa zinakuja kwenye Maabara Kuu kutoka nchi nzima mlitusaidia sana kupunguza mzigo wa upimaji sampuli zile baada ya nyinyi pia kuthibitika kuwa mnaweza kufanya kazi hii katika viwango vinavyokubalika".
Waziri huyo wa Afya alitembelea mabanda mbalimbali ya maonesho na kujionea teknolojia na mbinu mbalimbali za Kilimo,Mifugo na Uvuvi kabla ya kufunga rasmi maonesho hayo ya Wakulima nanenane Kanda ya Mashariki.
Akiwa kwenye banda la SUA alijionea vifaa mbalimbali vya maabara na wataalamu ambao walishiriki kwenye zoezi hilo na Upimaji wa sampuli za watu waliohisiwa kuwa na Ugonjwa wa COVID 19 sambamba na Hospitali pekee ya Taifa ya Rufaa ya wanyama iliyopo chuoni hapo.
Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo SUA kama Mdau Mkubwa wa Kilimo,Mifugo na Uvuvi kimeshiriki kwenye maonesho hayo Kitaifa Mkoani Simiyu na Kikanda kwenye Kanda ya Mashariki Mkoani Morogogoro




***Waziri wa Afya, Maendeleo ya jamii Jinsia wazee na watoto Mhe. Ummy Mwalimu akipata maelezo kwa mmoja wa Washiriki katika Maonesho ya Nane Nane alipotembelea Banda la SUA.***

# SUA yaibuka Mshindi Maonesho ya Nane Nane Kitaifa, 2020

Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo SUA Prof. Raphael Chibunda amewapongeza washiriki wote waliokitangaza Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo SUA katika Maonesho ya Wakulima Nanenane Kitaifa mkoani Simiyu na kupelekea SUA kushika namba moja kwa upande wa Vyuo Vikuu lakini pia SUA kushika namba tatu kwa ujumla katika maonesho ya Kanda ya Mashariki

"Mmefanya kazi kubwa sana niwapongeze kwa kushika nafasi ya kwanza hapa Simiyu lakini pia Morogoro tumeshika nafasi ya tatu kwa ujumla hongereni sana na tujipange mapema kwa maonesho yajayo, hongereni sana" alisema Prof. Chibunda






*Makamu wa Mkuu wa Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo SUA Prof. Raphael Chibunda (aliyeshika Kombe) akishangilian ushindi na washiriki wa SUA Nane Nane, Simiyu*

# Jaji Othman Chande afurahishwa na utendaji wa Prof. Peter Gillah

Jaji Mkuu Mstaafu ambaye pia ni Mwenyekiti wa Baraza la Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo SUA Mhe. Mohamed Othman Chande amempongeza aliyekuwa Naibu Makamu Mkuu wa Chuo (Taaluma) Prof. Peter Gillah kwa utekelezaji mzuri wa majukumu yake katika kipindi chake cha uongozi.
Mhe. Chande alitoa pongezi hizo wakati wa hafla fupi ya kumpongeza na kumtakia heri Prof. Gillah ambaye amestaafu wadhifa huo tarehe 30 mwezi 4 mwaka huu baada ya kutumikia nafasi hiyo kuanzia tarehe 1 Julai, 2011 ikiwa ni zaidi ya miaka 8
"Kuna sera nyingi za chuo ambazo Prof. Gillah ameshiriki katika uanzishwaji wake, kiukweli mchango wake ni mkubwa na unatambulika hapa chuoni, nimpongeze tu kwa ubunifu wake, uvumilivu wake na usikivu wake ambao leo hii umetufikisha hapa tulipo", alisema Jaji Mkuu Mstaafu Mh. Chande.
Awali akitoa salaam kwa wanajumuiya wa chuo, Makamu Mkuu wa Chuo hicho Pro. Raphael Chibunda amesema Prof. Gillah atakumbukwa kwa uchapakazi wake kwani alikuwa ni mtu jasiri, hodari na mwenye kusimamia majukumu yake.
"Prof. Gillah ni mtu ambaye akisimamia jambo basi ni kweli jambo hilo litatekelezeka, Profesa niwe mkweli nitakumiss sana kwani wewe ni mtu wa aina yake", alisema Prof. Chibunda.
Akizungumzia mafanikio yaliyopatikana chini ya uongozi wa Prof. Gillah, Rasi wa Ndaki ya Misitu,



*Prof. Peter Gillah akimkabidhi vitendea kazi na kumkaribisha Naibu Makamu Mkuu wa Chuo (Taaluma) mpya Prof. Maulid Mwatawala.*

*Inatoka Uk. 24*

Wanyamapori na Utalii Dkt. Suzana Augustino amesema Prof. Gillah amefanikiwa kuandaa na kutekeleza Mpango Mkakati wa Chuo wa kipindi cha miaka mitano kuanzia 2016/17 hadi 2020/21, kuongezeka kwa idadi ya wanafunzi kutoka 5,563 mwaka wa masomo 2011/2012 hadi kufikia wanafunzi 13,166 kwa mwaka wa masomo 2019/2020.

Mafanikio mengine ni kuongezeka kwa shahada za mafunzo yanayotolewa chuoni katika ngazi mbalimbali, kukiwezesha chuo kupata miradi mikubwa ya utafiti, upanuzi na ukarabati wa miundombinu mbalimbali pamoja na kukua na kupanuka kwa ushirikiano kati ya chuo na taasisi mbalimbali ndani na nje ya chuo.

Kwa upande wake Prof. Gillah amekishukuru chuo cha SUA kwa kutambua mchango wake huku akitoa wito kwa viongozi na wafanyakazi wa chuo hicho kufanya kazi kwa bidii na ushirikiano ili waweze kutekeleza ipasavyo majukumu yao na hatimaye waweze kufikia malengo ya Chuo.

Sherehe hiyo ya kumpongeza na kumtakia heri Prof. Gillah ilienda sanjari na kumuaga aliyekuwa Kaimu Naibu Makamu Mkuu wa Chuo Utawala na Fedha Prof. Yasinta Muzanila, kumkaribisha rasmi Prof. Amandus Muhairwa ambaye kwa sasa ndiye Naibu Makamu Mkuu wa chuo Utawala na Fedha pamoja na kumkaribisha Prof. Maulid Mwatawala ambaye ni Naibu Makamu Mkuu wa Chuo upande wa Taaluma



***Baadhi ya wageni mbalimbali waliohudhuria kwenye hafla ya kumpongeza na kumuaga aliyekuwa Naibu Makamu Mkuu wa Chuo (Taaluma) Prof. Peter Gillah***

# Prof. Mdoe atoa Baraka kwa SUA Kampasi ya Mizengo Pinda kuanza Udahili



*Naibu Katibu Mkuu Wizra ya Elimu, Sayansi na Teknolojia Mhe. Prof. James Mdoe akiongea jambo wakati alipotembelea Kampasi ya Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo iliyopo Mkoani Katavi mwezi Agosti, 2020. Katikati ni Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) Prof. Raphael Chibunda na Naibu Makamu Mkuu wa Kampasi hiyo upande wa Taaluum, Dkt. Anna N. Sikira.*

Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia Prof. James Mdoe ameridhishwa na maandalizi yaliyofanywa na Uongozi wa Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo SUA kwa ajili ya kuwapokea wanafunzi na kuanza rasmi kwa Kampasi ya Mizengo Pinda Mkoani Katavi.Prof. Mdoe aliyasema hayo wakati alipotembelea Kampasi hiyo mpya ya SUA iliyopewa jina la Waziri Mkuu Mstaafu Mhe. Mizengo Pinda alipokwenda kujionea maandalizi na mazingira ya Kampasi hiyo ambayo unatarajia kupokea wanafunzi tarehe 23/11/2020

Naibu Katibu Mkuu huyo amesema uanzishwaji wa Kampasi hiyo unasaidia jitihada za Serikali kupitia Wizara yake kwenye kuongeza nafasi nyingi zaidi za wanafunzi wenye sifa na wanaotaka kusoma elimu ya juu hasa baada ya maboresho makubwa ya elimu yanayofanywa na Serikali nchi nzima kwenye elimu ya Msingi na sekondari.

“ Kwanza niwapongeze sana SUA na uongozi mzima kwa kazi kubwa ambayo mmeshaifanya ya ujenzi na ukarabati wa majengo ya Kampasi hii, na sisi Kama Wizara tunawaahidi kuwasaidia ujenzi wa Bweni kubwa haraka ili Mwaka ujao wa masomo iwe imekamilika na itumike kuwezesha wanafunzi kuishi vizuri maana najua watakuwa wengi mwaka ujao” Alisema Prof. Mdoe.

Pia ametumia nafasi hiyo kuwashauri SUA kuanzisha

*Inatoka Uk. 26*

kozi fupifupi zitakazoweza kusaidia kuleta ujuzi kwa wananchi wa eneo hilo na Mkoa kwa ujumla ambazo hazihitaji mtu kuwa na sifa bali kutoa ujuzi kulingana na mahitaji ya wananchi hasa wale ambao hata hawajafika kidato cha nne.Naibu katibu Mkuu huyo awepongeza uzalendo Mkubwa aliouonyesha Waziri Mkuu Mstaafu Mhe. Mizengo Pinda kwa kuyatoa majengo hayo na Ardhi Kama shamba kwa ajili ya kuanzisha Kampasi hiyo na kuitaka jamii kuiga mfano huo wa aina yake kwa manufaa ya Umma.

Akitoa taarifa fupi ya Kampasi hiyo ya Mizengo Pinda Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo SUA Prof. Raphael Chibunda ameishukuru Serikali kwa jitihada kubwa ambazo inazifanya katika kuboresha mazingira ya kufundishia kuanzia Shule za msingi hadi Vyuo Vikuu na hivyo kuwezesha Watanzania wengi zaidi kupata elimu.

Prof. Chibunda alisema mara baada ya kukabidhiwa majengo hayo na Waziri Mkuu huyo Mstaafu Mhe. Pinda waliofanya tathmini na kutenga kiasi cha Shilingi Milioni 200 kwa ajili ya ukarabati lakini hadi kufikia hapa tayari wameshatumia kiasi cha Shilingi Milioni 810 na bado kazi inaendelea ili kuwezesha wanafunzi watakapoingia mazingira yote yawe tayari.Aliongeza kuwa Mtendaji Mkuu wa Tume ya Vyuo Vikuu alipata nafasi ya kumtembelea Kampasi hiyo yeye mwenyewe na alishukuru kuwa sasa wamepata ithibati ya kuanza kupokea wanafunzi kwa Mwaka huu kwa Kozi tatu maalumu kulingana na mahitaji ya Mkoa wa Katavi na mikoa mingine jirani.

“ Maono yetu kama Chuo ni kuona ukanda huu unakuwa na Chuo kikubwa na hivyo kuchochea Elimu na ujuzi kwa Wananchi badala ya wahitimu kwenda mbali kama Morogoro na Dar es salama kusoma Vyuo Vikuu, hapa ni mahali sahihi sana kwa kutolea



***Muonekano wa ndani wa moja ya Darasa katika Majengo ya Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) Kampasi ya Mizengo Pinda mkoani Katavi***

*Inatoka Uk. 27*

elimu pengine tofauti na maeneo mengine hivyo ni matumaini yetu kuwa vijana wa maeneo haya watakuwa wengi kuliko mikoa mengine" Alisema Prof. Chibunda.

Akizungumzia Kozi zitakazoanza kutolewa hapo Mkuu wa Kampasi hiyo Prof. George Mwamengele amesema wataanza na kozi tatu ambapo moja ni Astashahada ya Uongozaji watalii na Uwindaji salama, kozi ya pili ni Stashahada ya Kilimo na kozi ya tatu ni Shahada ya Nyuki na Mazao yatokanayo na Nyuki.

Prof. Mwamengele amesema maandalizi kwa kiasi kikubwa yamekamilika kwa maana ya miundombinu kama vile madarasa, Mabweni, Mifumo ya Mtandao lakini pia Chuo kimeajiri walimu wapya wa kutosha na wengine wakongwe wamehakikishiwa Kampasi hiyo kutoka SUA kampasi kuu Mkoani Morogoro.

Dirisha la maombi kwa wanafunzi wa kozi mbalimbali kwenye Kampasi Kuu na kampasi hii mpya ya Mizengo Pinda litakuwa wazi kuanzia tarehe 31/08/2020 na Wanafunzi kwa mujibu wa kalenda ya masomo wanatakiwa kuwasili Chuo kwa ajili ya kuanza masomo tarehe 23/11/2020.




***Naibu Katibu Mkuu Wizra ya Elimu, Sayansi na Teknolojia Mhe. Prof. James Mdoe (wa pili kulia)akiwa kwenye picha ya pamoja na Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo Prof. Raphael Chibunda (wa kwanza kulia), Mkuu wa Kampasi ya Mizengo Pinda Prof. George Mwamengele (wa kwanza kushoto) pamoja na Naibu Makamu Mkuu wa Chuo (Taaluma) Kampasi ya Mizengo Pinda Dkt. Anna N. Sikira, wakati alipotembelea Kampasi hiyo Mwezi Agosti, 2020.***

# Imetolewa na:
# Idara ya Mawasiliano na Masoko
# SUA

*S.L.P. 3000 CHUO KIKUU, MOROGORO, TANZANIA*
*Simu: 255-023-2640006/7/8/9,*
*Barua pepe: communicationandmarketing@sua.ac.tz*